



Safiri na Treni ya Deluxe sasa kwa Tshs. 60,000 tu kwa Daraja la Pili ukiwa umelala

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Nd. Masanja Kadogosa akijandikisha kwenye kitabu cha wageni alipotembelea banda la Shirika la Reli Tanzania kwenye Maonesho ya Wakulima-Nanenane katika viwanja vya Nyakabindi wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu tarehe 08/08/2018.



Mkurugenzi wa Idara ya Ishara na Mawasiliano Mhandisi Felix Mutashobya (kushoto) akikabidhi Vifaa vya mawasiliano (VHF) 5 kwa Meneja wa mizigo na usafirishaji Bwana Shabani Kiko (kulia) katika ukumbi wa TRC ili vifaa hivyo vitumike katika vivuko vya Nkuruma, Kamata, Kawawa, Buguruni, na Vingunguti kwa ajili ya kusaidia kupunguza na kuzuia ajali kwenye vivuko vya Reli tarehe 31 Julai 2018.

Timu ya Mawasiliano kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC ikitoa elimu kuhusu miradi ya SGR na TIRP inayoratibiwa na kusimamiwa na TRC, faida, changamoto na mambo ya kuzingatia wakati wa ujenzi na uboreshaji wa reli ya katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bwana Komani Kitwala katika ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Tabora Mjini Agosti 2018.



Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Huduma zitolewazo na TRC Bwana Focus Sahani (wa kwanza kulia), wahandisi wa TRC, Maofisa kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Fedha wakipata maelezo kutoka kwa Mhandisi wa Yapi Merkezi (wa pili kulia) walipotembelea kambi za SGR za Ilala, Soga na Ngerengere kuona maendeleo ya mradi wa ujenzi wa SGR mnamo tarehe 06/08/2018.



Mhandisi kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC Bwana Prosper Tweve (wa kwanza kushoto) akitoa elimu kuhusu miradi inayosimamiwa na TRC kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Biashara iliyopo Bariadi mkoani Simiyu walipotembelea Banda la TRC katika Maonesho ya Wakulima - Nanenane kwenye viwanja vya Nanenane Nyakabindi wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu tarehe 07/08/2018.